

SURA YA PILI

Na wakati huu kelele za nguvu ziliongezeka na ndipo Venia anaamua kutoka nje huku ameshikilia kandambili moja mkononi. Anatembea kwa kasi kuelekea eneo la tukio na kupenya katikati ya kundi kubwa lililojaa watu. Venia anapenda sana matukio, na kwake hekaheka na fujo za mtaani za mara kwa mara ndio burudani tosha kuliko chochote kile. Anakazana kukodoa macho na ndipo anapomuona binti mmoja akiwa katikati ya umati huo huku akijaribu kujitetea jambo. Baada ya Venia kugundua kinachoendelea ndipo alipojisemea “Binti mrembo namna hii, kweli amekosa nauli ya kumlipa bodaboda hadi anaaibishwa hivi!!...” Anajiuliza huku akiwatazama vijana wengi wanaoonekana kumshambulia kwa maneno na vipigo binti huyo. Ghafla watu wote wanakimbia na kutawanyika ovyo baada ya uongozi wa mtaa kutokea na kutaka kuwadhibiti vijana hao wanaojichukulia sheria mkononi. Ndipo Venia anaamua kurudi nyumbani kwake na ghafla anagundua amepoteza kandambili aliyokuwa ameishikilia mkononi pamoja na kofia ya kulalia aliyokuwa amevaa kichwani.

SURA YA TATU

Ndipo anaanza kujikagua na kugundua amekurupuka bila kunawa uso na hivyo anapaswa kurudi nyumbani na kujiweka sawa. Anafika na kusukuma mlango na ndipo anagundua aliegesha tu mlango bila kufunga katika mishemishe za kukimbilia kelele zilizotokea muda mfupi uliopita. Anaingia na kujilaza kitandani huku akichezeachezea simu yake ya mkononi aliyokuwa ameiweka chini ya mto. Anapekuu mitandaoni kwa dakika kadhaa na ndipo anashituka baada ya kupiga miayo inayoashiria njaa kwani ni takribani saa tano kasoro hajaweka kitu mdomoni. Anakwenda kupiga mswaki na kuoga tayari kwa kuandaa chai. Huwezi kuamini kama ni Venia aliyekurupuka bila kunawa wala kuvala kandambili ili kushuhudia ugomvi masaa machache yaliyopita. Kwani amevalia vizuri blauzi yake na kanga kwa ajili ya kuingia jikoni kushughulikia tumbo lake. “Ntakuja huko jioni shost si unajua mimi sипитви na jambo”...Alisikika akizungumza baada ya kupokea simu aliyoiveka loud speaker huku ameshikilia kipande cha mkate na kikombe cha chai mkononi.

SURA YA NNE

“Eeeeh, Venia anaendelea kuzungumza na simu huku akinywa chai yake taratibu. Venia ni binti mwenye umri wa miaka 27 na ni mtoto pekee wa kike katika familia ya Mzee Mafute anayeishi mtaa wa Mombo hapa Jijini. Ni binti wa mwisho kuzaliwa ambaye ana kaka zake watatu na wote wameoa. Venia alibahatika kusoma na kuishia kidato cha nne baada ya kufeli na kushindwa kuendelea na masomo ndipo alipoamua kuishi mwenyewe na kuanza kujitegemea. Mishemishe ni nyingi mjini lakini Venia hajui wapi pa kuanzia. Ni siku nyingine Venia anaamka mapema na kuijandaa kuelekea kanisani kwani alisikia kuna maombi yanafanyika na watu wenyе shida mbalimbali wataombewa. “Inawezekana na mimi ntapata kazi.” Anajisemea huku anachukua Biblia kisha anaifunua kidogo na kuiweka kwenye pochi, ndipo anapoanza kupiga chafya kali mfululizo na kugundua imejaa vumbi kutokana na kutotumika kwa muda mrefu.

SURA YA TANO

Venia anafika kanisani na kutafuta sehemu ya kukaa mara anapokelewa na muhudumu mmoja akimuelekeza sehemu ya kukaa, anaelekea alipoelekezwa huku akishusha polepole siketi yake iliyokuwa fupi kiasi. Venia anakaa Jirani kabisa na binti ambaye kimtazamo anakadiriwa kulingana naye umri. Anakosa utulivu binafsi na kujikuta anashangaa ovyo ukizingatia huwa hana kawaida ya Kwenda kanisani mara kwa mara. “Sijui niende kukaa pale mbele kabisa?” Anajisemea huku anainuka kidogo kuashiria kutafuta sehemu nyingine. Mara anatazama pembedi na kumuona Jirani yake akiwa anafanya maombi binafsi kwa sauti ya chini huku ameshika Biblia. Anakumbuka na yeye ameweka Biblia yake kwenye pochi, mara anaitoa na kuifunua upesi hata asijue anafunua nini. Mara anasikia pambio lililomfanya asimame na kucheza. Ghafla anaacha kucheza na kutazama vijana waliovalia sare vizuri wakiingia ndani kwa furaha. Ni muda mfupi usio na utulivu kwa Venia kiasi cha muumini yejote kugundua kwa wepesi kuwa ni mgeni katika kanisa hilo.

SURA YA SITA

Ibada inakwisha lakini kwa Venia inakuwa tofauti sana kwani muda mwingu ameutumia kuwashangaa watu waliokuwa wanaingia na jinsi walivyovalia. Miezi kadhaa imepita sasa, Venia anakosa msimamo mzuri wa kuendesha Maisha yake kwani mtaji wa kuendeleza biashara yake ndogo ya dagaa wa kukaanga umetumika hivi karibuni baada ya kulipia kodi ya nyumba na kubaki bila kitu. Akiwa katika Mawazo mazito, mara simu yake inaita. “Hallo....ndio....Unasema?....ndio....Nashukuru sana....”Anakata simu na kushangilia huku akichezacheza kwa furaha. Venia alipokea simu ikimtaka kuwasili kazini siku ya Jumatatu baada ya kufanya usahili muda mrefu takribani miezi mitano iliyopita. Ni katika kampuni ya usafi ambayo imeajiri vijana zaidi ya 500 katika ofisi mbalimbali za umma na binafsi. Venia anamwaga nguo zake zote chini na kuanza kuchambua nguo mojamoja huku akichagua nguo ya kuvaa siku hiyo ya jumatatu. Anajiuliza huku akivaa na kuvua nguo tofautitofauti na kuchezacheza kwa furaha.